# Mwongozo wa Ufuatlilaji wa watu waliotangamana na waathiriwa wa COVID-19

Waraka huu umeandaliwa kuleta ufafanuzi kusaidia Mashirika ya Kitaifa katika kufanya maamuzi ya jinsi ya kusaidia mkakati wa serikali zao katika ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa kama sehemu ya mpango wa kukabili COVID-19. Kutokana na utata wa COVID-19, mawanda yake ya duniani, vipaumbele vya taifa na uwezo wa Mashirika ya Kitaifa, ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa unaweza kuwa njia moja ya kujumuisha kwenye mpango wa makabilio. Waraka huu unatoa muongozo wa maamuzi iwapo usaidizi katika ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa unafaa, pamoja na mambo ya kuzingatia kuyaweka ndani ya mipango ya ufuatiliaji waliotangamana na waathiriwa.

## Yaliyomo


Yaliyomo ..... 1

Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa: Nini na Kwa nini ..... 2

Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa ukilinganishwa na njia nyingine za uchunguzi wa afya ya jamii ..... 2

Nani aliyetangamana na waathiriwa? ..... 3

Mazingatio ya jumla katika ufuatiliaji waliotangamana na waathiriwa ..... 4

Ufafanuzi wa kisa cha COVID-19 ..... 5

Utekelezaji wa ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa wa COVID 19 ..... 6

Mbinu Zilizopendekezwa ..... 6

Mpangilio kwa ujumla na Mahitaji ya Uratibu ..... 7

Usalama wa Aliyejitolea ..... 8

Vitu vya Kufanya na Kutofanya katika Ufuatiliaji ..... 9

Viashiria vilivyopendekezwa katika Kufuatilia na Kutathmini Utekelezaji wa Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa ..... 10

ZANA ZA ZIADA NA MWONGOZO ..... 10

## Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa: Nani, Nini na Kwa nini

Ufuatiliaji waliotangamana na waathiriwa ni mchakato wa kutambua, kukadiria na kudhibiti watu ambao wamekaribia virusi vya COVID-19 kuzuia kuendelea kuenea. Watu ambao wamekaribia virusi vya COVID-19 hufuatiliwa kwa siku 14 mfululizo kuanzia siku waliokaribiana na virusi hivi karibuni. Tafadhali zingatia kwamba siku 14 zimependekezwa na WHO, lakini baadhi ya serikali zinaweza kuwa na matakwa yao. Tafadhali hakikisha kuwa Shirika la Kitaifa linafuata matakwa ya Serikali ya Kitaifa na maafisa wa afya.

Mchakato huu utasaidia kutambuliwa kwa haraka kwa watu wanaoonyesha dalili kwa kuwafualitia wale wanaoweza kupata dalili (watu wa karibu). Kuwatambua watu katika mwanzo wa dalili na kuwatenga kunapunguza watu wengine kukaribia virusi, kuzuia kutokea kwa maambukizi. Utengaji wa haraka na kumlaza mtu mwenye dalili kwenye kituo cha afya au kituo cha tiba kunapunguza ucheleweshwaji wa tiba inayostahili, ambayo ingeweza kuimarisha uwezekano wa kupona.

### Ufuatiliaji wa watu waliotangamana na waathiriwa ukilinganishwa na njia zingine za uchunguzi wa afya ya jamii:

Kuna njia nyingi za kujumusiha aina tofauti za uchunguzi na ugunduzi katika Mashirika ya Kitaifa, na ufutiliaji wa waliotangamana na waathiriwa ni njia moja kati ya hizo.

| Mchakato | Madhu muni | Nani | Kivipi |
|---|---|---|---|
| **Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa** | Utambuzi na ufuatiliaji wa watu ambao wanaweza kuwa wamekuwa karibu na mtu mwenye maambukizi ya COVID-19 | Wafanyakazi wakujitolea katika vituo vya afya walipata mafunzo (waliojitolea katika Shirika la Kitaifa wakihitajika) kwa maombi maalumu, ushirikiano na mafunzo kutoka kwa serikali ya kitaifa au serikali za mitaa | Watu wakaribu kutengwa na kufuatiliwa kwa siku 14 baada ya uwezekano wa kukaribiana na virusi. Hii inajumuisha:<br>1. Kupata watu wanaoafiki ufafanuzi wa watu wa karibu, na<br>2. Ufuatiliaji iwapo watu wao wataonyesha dalili (kwa simu kila siku ikiwezekana) |

IFRC

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Kutafuta visa vya wagonjwa** | Kutafuta kwa mpangilio na kupima virusi vya COVID-19 ndani ya kundi lengwa au sehemu zinazoaminika kuwa hatari | Wanaepidemiolojia, wafanyakazi wa afya katika jamii au wengine kulingana na uwezo wa mfumo wa afya | Wanahitaji uwezo wa haraka wa upimaji na rasilimali watu, inaweza kujumuisha vituo vya upimaji, nyumba kwa nyumba, au utafutaji ndani ya wodi za hospitali kwa watu ambao wamekosea kupimwa |
| **Upimaji Mipakani** | Upimaji ambao unafanyika katika sehemu za mipaka au sehemu zilizodhibitiwa kukadiria iwapo kuna dalili kwa wasafiri | Maafisa wa serikali (Wafanyakazi wa afya, wanajeshi, polisi, nk.), kulingana na wajibu wanaweza pia kutoka kwa RCRC NS | Kulingana na mahitaji ya serikali ya Kitaifa. Upimaji wa dalili kulingana na WHO au ufafanuzi wa Kitaifa wa visa |
| **CBS** | Utoaji wa taarifa maramoja wa hali hatarishi ya kiafya unaolingana na Vigezo vya COVID-19 kama vilivyofundishwa wakati wa shughuli za uhamasishaji wa afya zinazolingana na vigezo vilivyoteuliwa | Watoa huduma wa kijamii waliopata mafunzo katika Shirika la Kitaifa | Wanaojitolea wanaweza kutoa taarifa hatarishi za kiafaya zinazolingana na COVID-19 |
| **Namba ya dharura ya Kutoa taarifa** | Mfumo wa mawasiliano unaoruhusu wanajamii kupiga simu na kutoa taarifa ikiwa wanaamini kuwa COVID-19 ni suala katika jamii yao na kutoa taarifa kuhusu dalili kwa ufuatiliaji | Wanajamii, wafanyakazi wa vituo vya afya, wanaojitolea kutoka RCRC (watu/jamii) | Inahitaji namba ya dharura ya taifa au mtaa kuanzishwa na kutunzwa kwa ajili ya kuunganisha rufaa |

## Nani aliyetangamana na waathiriwa?

*Ufafanuzi wa WHO wa"nani aliyetangamana na waathiriwa" ulioelezwa hapa chini na unafaa kutumika na/au kurekebishwa kulingana na matakwa maalumu ya Wizara ya afya kama kunautofauti.*

Aliyetangamana na mwaathiriwa ni mtu aliyepitia mojawapo ya kukaribia virusi kati ya siku 2 kabla na siku 14 baada ya dalili kuanza za kisa kinachoshukiwa au kuthibitishwa:

1. Kukutana uso kwa uso na kisa kinachoshukiwa au kuthibitishwa ndani ya mita 1 na kwa zaidi ya dakika 15;

2. Kutangamana na moja kwa moja na kisa kinachowezekana au kilichothibitihswa;
3. Kumtunza mgonjwa wa COVID-19 anayeshukiwa au kuthibitishwa bila kutumia vifaa sahihi vya kujikinga; AU
4. Hali nyingine kama inavyoashiriwa na thamini ya hatari mtaani.

Kumbuka: kwa visa vilivyothibitishwa bila kuwa na dalili, kipindi cha mtu kutangamana hupimwa kama siku 2 kabla hadi siku 14 baada ya tarehe ambayo sampuli zilichukuliwa ambazo zilipelekea kuthibitishwa.

## Mazingatio ya ujumla katika kufuatilia waliotangamana na waathiriwa[1]:

Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa unategemea ushirikishwaji na ushirikiano kutoka kwa jamii zilizoathirika ili kuweza kuwa na ufanisi. Kujenga mahusiano ya kuaminiana, kila jitihada zinatakiwa zifanywe kushirikisha jamii, kuelezea nia na mchakato kwa ufasaha na kujibu maswali au wasiwasi watu wanaoweza kuwa nao.
Jamii zinatakiwa ziweze kujiamini kushirikiana na timu ambazo zinaongoza ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa.

Ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa hufanyika vyema katika hali mawasilano ya njia mbili yanayofaa, sahihi na yanayoheshimu utamaduni. Uandikishaji wa waliotangamana na waathiriwa unategemea utayari wa jamii kufuatiliwa; wanaweza kuwa na utayari zaidi au kidogo kuweza kufuatiliwa kulingana na uelewa wao wa COVID-19, uwezekano wa unyanyapaa[2] unaohusishwa na kutangamana na mwathiriwa (kutoka kwa wenzao, familia, au jamii), na jinsi wanavyojisikia kwa ujumla kuhusu COVID-19. Watu pia wanaweza wasitake kutambuliwa au kugundulika ikiwa kutakuwa na vizuizi kazini au shuleni, na wanaweza wasitake kutoa taarifa za watu wengine waliotangamana na waathiriwa kwa sababu ya unyanyapaa na uwezekano wa kulipiza kisasi. Umma kuelewa vibaya na mtazamo kuhusu orodha ya waliotangamana na waathiriwa kuonekana kama ni orodha ya watu ambao wanaweza kufa inaweza kusababisha upinzaji katika jamii na kuzuia ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa. Kwa hivyo, mawasiliano ya kiafya na utumaji wa ujumbe na msaada wa kisaikologia unaotolewa kwa jamii ni muhimu. Mikakati ifuatayo inaweza kukuza ushirikishwaji wa jamii na kuepuka unyanyapaa:

- Shirikisha na uelimishe viongozi wa jamii kuhusiana na maambukizi,kusambaa kwa COVID-19 na hatua ambazo jamii zinaweza kuchukua ili kuukabili, ikiwemo umuhimu wa kufuatiliwa kwa waliotangamana na waathiriwa.
- Shirikisha maeneo ya kidini kama vile makanisa na misikiti, kutoa maelezo kamili kwa jamii (kama yako wazi na yameidhinishwa na Wizara ya Afya) ikiwemo kueleza mbona kufuatiliwa kwa waliotangamana na waathiriwa kunafaidi jamii nzima.
- Tumia mawasiliano ya kiafya mapema na juhudi za elimu, ikiwezekana kabla ya mwanzo wa COVID-19.
- Sikiliza na ujibu maoni ya jamii, ikiwemo hofu zozote na wasiwasi ambao watu wakonao kuhusu kufuatiliwa kwa waliotangamana na waathiriwa, na uhakikishe zinanakiliwa, zinachambuliwa na kujibiwa.
- Tumia msaada wa kisaikologia wa mapema ili kuondoa hofu inayohusiana na COVID-19.
- Elimisha jamii kuhusu umuhimu wa usiri wa visa vya walioathirika na waliotangamana nao.
- Kuna zana nyingi za mawasiliano ya hatari na za ushiriki wa jamii (RCCE) ambazo zinaweza kusaidia vitendo vilivyotajwa hapo juu, zikiwemo asilimali za mafunzo, zana za maoni,na mwongozo wa mfanyakazi wa jamii na unyanyapaa. Unaweza ukapata zana hizi zote hapa.

Kufuatiliwa kwa mafanikio waliotangamana na waathiriwa kunahitaji ujuzi katika tathmini ya dalili za COVID-19, mbinu za mahojiano na ushauri nasaha. Waliojitolea wanahitaji kuwa na uwezo wa kubadilika na kuwa na huruma kwa walioathirika, waliotangamana nao na familia ili kujenga uaminifu na uhusiano mzuri na jamii.

[1] Imebadilishwa kutoka: Miongozo ya Dharura: Implementation and Management of contact tracing for Ebola virus disease (WHO, CDC)
[2] Kwa mwongozo zaidi juu ya jinsi ya kushughulikia unyanyapaa unaohusiana na COVID-19 tazama "A Guide to preventing and addressing social stigma" ulioandaliwa na IFRC, UNICEF na WHO.

Watekelezaji wa shughuli za kufuatiliwa kwa waliotangamana na waathiriwa unalingana na uzito wa ugonjwa huo na muktadha wa kijmaii. Idadi za visa na waliotangamana nao zinazopatikana kila siku zinaweza kujumuisha maeneo mengi ya kijografia kama vile maeneo ya mijini yenye watu wengi, ikitoa changamoto za kupatikana kwa wale waliotangamana na waathiriwa. Katika hali kama hizi, kamili na mfumo shughuli za kufuatiliwa kwa waliotangamana na waathiriwa zinahitaji kuimarishwa kupitia ushiriki thabiti wa jamii na uhamasishaji wa jamii.

Kabla RCV watekeleze ufuatiliaji wa waliotangamana na waathiriwa na serikali za mitaa au kitaifa, ni muhimu kukagua taarifa zozote au makubaliano ya waliojitolea ili kuhakikisha kuwa zinajumuisha kifungu kinachokataza kufichua habari za kibinafsi, za siri au ujumbe nyeti. Rekodi ya saini inapaswa kuwepo kwa waliojitolea wanaoshiriki kutafuta waliotangamana na waathiriwa. Inapaswa kuwekwa wazi katika mafunzo kwamba kufichua habari za kibinafsi, ya siri au nyingine nyeti, haswa kulingana na kazi ya CT inaweka usalama wa watu katika hatari na hivyo inakatazwa kabisa. Aidha, inapaswa kuwekwa wazi kutoka kwa maafisa wa serikali ikiwa RCV wanaweza kuwekwa jukumu katika mchakato wa CT. Waliojitolea wanafaa kuelezwa kuwa wanaweza hitajika kutia saini tarifa za ziada za usiri ikiwa watafanya kazi moja kwa moja na Wizara ya Afya au mamlaka ya serikali.

## Ufafanuzi wa kisa cha COVID-19

Ufafanuzi kisa uliopendekezwa na WHO[3] ulioelezwa hapa chini unafaa kulinganishwa na kubadilishwa katika kila nchi kuafikiana na matakwa na Wizara ya Afya (ikiwa ipo).

Kisa kinachoshukiwa ni :

**A.** Mgonjwa aliye na maradhi makali ya mfumo wa kupumua (joto jingi na angalau ishara/dalili ya maradhi ya mfumo wa kupumua, kama vile, kikohozi, matatizo ya kupumua), NA historia ya kusafiri au kuishi katika eneo linaloripoti maenezi ya ugonjwa wa COVID-19 katika jamii wakati wa siku 14 kabla ya dalili kuanza;

AU

**B.** Mgonjwa aliye na maradhi makali ya mfumo wa kupumua NA ambaye ametangamana na mtu ambaye amethibitishwa au anashukiwa kuwa na COVID-19 (tazama ufafanuzi wa waliotangana na waathiriwa hapa chini) ndani ya siku 14 kabla ya dalili kuanza

AU

[3] Tafadhali zingatia kuwa Tovuti ya Ukadiriaji wa Kidunia wa maambukizi ya virusi vya korona kwa binadamu inaeleza sasisho ya mwisho tarete 27 Februari, 2020, ingawa PDF inayoweza kupakuliwa inaendelea kuwa na habari iliyosasishwa - kwa mujibu wa makala haya yalisasishwa tarehe 20 Machi 2020. Kabla ya kuanza shughuli za ufatutaji watu waliotangamana na waathiriwa, tafadhali hakikisha una ufafanuzi wa kisa wa hivi karibuni kutoka kwa Wizara ya Afya au WHO.

**C.** Mgonjwa aliye na maambukizi makali ya mfumo wa kupumua (kama vile joto jingi, na angalau ishara au dalili moja ya maradhi ya mfumo wa kupumua, kwa mfano kikohozi au matatizo ya kupumua NA anayehitaji kulazwa hospitalini) NA katika ukosefu wa utambuzi mbadala unaoeleza dalili zake.

Kisa **Kinachowezekana** ni:

A. Kisi kinachoshukiwa ambacho upimaji wa virusi vya COVID-19 kinajumuisha; AU

B. Kisa kinachoshukiwa ambacho upimaji haukuweza kutekelezwa kwa sababu yoyote.

Kisa **Kilichothibitishwa** ni:

Mtu aliye na maambukizi ya COVID-19 yaliyothibitishwa kwa maabara, bila kujali ishara na dalili.

## Utekelezaji wa utafutaji wa watu waliotangamana na waathiriwa wa COVID-19

Wanaotafuta watu waliotangamana na waathiriwa wanafanya kazi kutambua watu wa jamii, familia, kazi na wafanya kazi wa afya ambao wametangamana na mtu aliyethibitishwa kutoka siku 2 kabla ya dalili kuanza na hadi siku 14 baada ya kuanza kwa dalili zao au kadri dalili zao zinavyozidi ikiwa ni zaidi ya siku 14. kuunda orodha, ikujumuisha habari za kidemografia, tarehe ya kwanza ya kutangamana au tarehe ya kutangamana na kisa kilichothibitishwa au kisa kinashowezekana, na tarehe ya kuanza kwa dalili za mfumo wa kupumua. Watu waliotangamana na waathiriwa na aina ya utangamano na kisa kilichothibitishwa au kinachowezekana wanafaa kunakilishwa vilivyo kwa mtu yeyote atakayeambukizwa na COVID-19, kulingana na mwongozo na taratibu za Wizara ya Afya.

Kwa waliotangamana na waathiriwa wa kisa cha COVID-19 kinachoshukiwa, angalau, RCVs wanafaa kuhimiza usafi wa mikono na mfumo wa kupumua na wanaweza kuhimiza - kwa mujibu wa muktadha wa epidemiolojia na rasilimali zilizoko, pamoja na sera ya Wizara ya Afya- kijufuatilia kwa dalili, kukaa mbali na watu au kujitenga.

### Njia zilizopendekezwa

Ili kubainisha mawanda na mahitaji ya utafutaji watu waliotangamana na waathiriwa wa COVID-19 tafadhali hakikisha umewasiliana na mhusika katika Wizara ya Afya. Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (MoHCDGEC) itakuwa na itifaki maalum inayoendana na mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na mbinu zilizopendekezwa hapo chini lakini itarekebishwa ili kukidhi mahitaji katika muktadha wao maalum. Usalama wa Watu wa Kujitolea ni muhimu na unapaswa kushughulikiwa katika itifaki ya MoHCDGEC. Mapendekezo kadhaa yameorodheshwa hapa chini pamoja na ugavi wa jumla wa vifaa na uzingatiaji wa Rasilimali Watu.

Mpangilio wa Jumla na Mahitaji ya Ugavi wa Vifaa

| Aina | Mapendekezo ya Kuzingatia | Ndiyo / Inaweze kana | Hapana / Haiweze kani kwa sasa |
|---|---|---|---|
| Mpango/ Michakato ya Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika | 1. Itifaki ya Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika iliyopangwa na washirika/ MoHCDGEC, wadau husika<br>2. Wajibu na majukumu kwa RCVs (Watu wa Kujitolea kwa ushirikishwaji thabiti wa jamii) yamefafanuliwa wazi<br>3. Mkakati wa RCCE (Mawasiliano ya hatari na ushirikishwaji wa jamii) na PPS izingatiwe katika mchakato wa kupanga<br>4. Kagua mikataba ya usiri ya W na hakikisha wanafaa na wapo tayari kwa ajili ya Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika | | |
| Rasilimali Watu inayopendekezwa | Afisa 1 wa Wilaya (au sawa yake) kwa kila eneo<br><br>Msimamizi Ana 1 kwa Watu wa Kujitolea 20-30 (Wasimamizi wanaweza kuwa maafisa wa MoHCDGEC, Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii/ CHWs, au sehemu ya RCRC)<br><br>Mtu wa Kujitolea 1 kwa Watu waliokaribiana na Aliyeathirika 20-30 | | |

IFRC

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mambo ya Kuzingatia kuhusu Ugavi wa Vifaa | Usafiri / Ufikiaji wa Jamii ikiwa inahitajika katika mazingira ya eneo<br><br>Hali ya usalama katika maeneo husika<br>• Wafanyakazi wa Kujitolea wanaweza kutembea ndani ya jamii na kufanya shughuli, AU Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika anafikiwa kwa simu<br>• Ziara za usimamizi zinawezekana<br>• Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika kunakubalika na jamii<br><br>Mfumo wa Kufuatilia Mtu Aliyejaribiana na Aliyeathirika kwa msingi wa kimaandishi:<br>• Fomu zilizochapishwa kwa Watu wa Kujitolea<br>• Vitabu vya ripoti kwa wasimamizi<br><br>Teknolojia zinazotegemea Programu za kidijitali<br>• Simu janja na mtandao unapatikana kwa wasimamizi kulingana na mpango wa Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika<br><br>Usafi<br>• Watu wote wa Kujitolea wanaofanya kazi ya Kufuatilia Watu waliokaribiana na Aliyeathirika wanapaswa kupata huduma ya vitakasa mikono na/ au kunawa mikono | | |
| Mafunzo Yanayopendekezwa | Mafunzo ya Watu wa Kujitolea katika kila eneo<br>• Msimamizi wa kituo kuongoza<br>• Imependekezwa isizidi 25<br><br>Siku 2-4 za mafunzo ya Watu wa Kujitolea juu ya Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika, pamoja na RCCE.<br><br>Mafunzo ya marudio kama yanahitajika | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ufuatiliaji, Tathmini na Utaratibu wa Kutoa Mrejesho | • Viashiria vya msingi vinazingatiwa na vinaweza kupimwa endapo kuna rasilimali zinazotarajiwa<br>• Utaratibu wa Kukusanya Maoni ya Jamii ni pamoja na<br>kusanya na chambua mawazo ya watu, hofu, maswali na maoni juu kuhusu Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika na COVID-19 kwa ujumla. Ikiwa maoni pia yanakusanywa kupitia shughuli zingine kama uhamasishaji wa kijamii, hii inapaswa kujumuishwa hapa na mfumo mmoja wa jumla kwa Jamii ya Kitaifa. | | |

## Usalama wa Watu wa Kujitolea

Ikiwezekana, inashauriwa kufanya kazi ya Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika kwa simu. Hii inaruhusu kiwango cha juu cha ulinzi kutoka kwa maambukizi yanayowezekana na pia faragha ya kibinafsi. Lakini, katika hali nyingi kufuatilia kwa simu haiwezekani. Ikiwa ufuatiliaji wa binafsi unahitajika, mapendekezo ya chini yanashauriwa kwa utendaji bora.

Watu wa Kujitolea wote, katika Hali ya kila ngazi ya maambukizi wanapaswa kupata huduma ya kitakasa mikono baada ya kila
ziara ya kibinafsi. Inapendekezwa kwamba **Watu wa Kujitolea wote wawe umbali wa mita 1-2** kutoka kwa wanajamii wakati wa majadiliano na **hakuna kugusana mwili** kunapaswa kufanyika. Ikiwezekana, majadiliano yanapaswa kufanyika nje, kupitia dirisha au katika eneo la wazi na kati ya mtu mzima wa familia / mtu wa jamii na Mtu wa Kujitolea badala ya mgonjwa mwenyewe.

Ikiwa Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika kunafanywa na "CHV"(Community Health Volunteers) ambao wamefunzwa kutoa msaada wa ziada wa afya, wanapaswa kufuata hatua zozote za "PPE" (Personal Protective Equipment) zinazohusiana na shughuli hizo na masharti ya serikali.

Watu wa Kujitolea wanaofanya shughuli za Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika hawahitaji kuvaa PPE. Kuvaa barakoa au glavu haipendekezwi, kwani inachangia hofu katika jamii, husababisha hisia za zisizofaa za usalama, na sio lazima kwa sababu ya tahadhari za umbali wa kimwili. Lakini, ikiwa mwongozo wa MoHCDGEC ni kuvaa PPE wakati wa Kufuatilia Watu waliokaribiana na Aliyeathirika, tafadhali fuata mwongozo wao na hakikisha kupokea PPE za kutosha kutoka kwa wasambazaji ya MoHCDGEC.

Vitu vya Kufanya na Kutofanya wakati wa Kufuatilia Watu waliokaribiana na Aliyeathirika

**FANYA**

- Dumisha umbali wa kimwili unaofaa na kupiga simu inapowezekana kukamilisha kazi ya Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika
- Uwe mwenye huruma, sikiliza na ujibu wasiwasi wa wale unaowasiliana nao na utumie maarifa yako kwenye "RCCE"(Risk Communication and Community Engagement), "PSS" na stadi za usaidizi uliopata katika mafunzo ya Watu wa Kujitolea
- Zingatia maoni ya jamii ukitumia mwongozo na zana za IFRC na RCCE Ongea na RCC wa Jumuiya ya Kitaifa na CEA wa mahali ambako watu wengi hukutana.
- Osha mikono yako na sabuni na maji, au tumia kitakasa mikono baada ya kila ziara
- Mfikie msimamizi wako ikiwa hauna uhakika au unajihisi haupo salama wakati wowote.
- Fuata taratibu zote za usalama zilizowekwa na Jumuiya ya Kitaifa na Serikali.

**USIFANYE**

- Kunyanyapaa watu au kuwafanya waone aibu kwa mahitaji ya kufuatwa
- Kujadili majina au taarifa ya za Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika nje ya juhudi za mpango wa Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika
- Kuingia katika nyumba wakati unafanya shughuli za Kufuatilia Mtu Aliyekaribiana na Aliyeathirika, watu wa Kujitolea WANAPASWA kuzungumza na watu nje au kupitia dirisha, kutunza umbali wa mita 1-2.
- Usimguse au kuwa karibu zaidi ya mita 1 na mtu yeyote.
- Kukasirika, Watu Wanaojitolea WANAPASWA kuwa wavumilivu na kusikiliza maswala na kutoa taarifa sahihi ili kupinga uwongo au uvumi.

Viashiria vilivyopendekezwa vya Kusimamia na Kutathmini utekelezaji wako wa kufuatilia watu waliokaribiana na aliyeathirika

| Kiashiria kinachopendekezwa | Mahesabu / Maelezo | Madhumuni |
|---|---|---|
| % ya idadi ya watu waliokaribiana na aliyeathirika uliowatembelea/ kuwasiliana nao kwa siku | # ya watu waliokaribiana na aliyeathirika kwa siku uliowatembelea, au kuwasiliana nao / Lengo # la watu Waliokaribiana na aliyeathirika uliowatembelea, au kuwasiliana nao | Ufuatiliaji |
| % ya visa vinavyoshukiwa au vilivyothibitishwa katika maeneo lengwa yaliyotajwa na kugundulika kupitia shughuli za kufuatilia Watu Waliokaribiana na aliyeathirika za RCV | # ya visa vilivyothibitishwa vilizotajwa kupitia njia ya RCV kufuatilia Watu Waliokaribiana na aliyeathirika kwa mamlaka / Jumla ya # ya visa vilivyothibitishwa na mamlaka katika maeneo yaliyolengwa | Matokeo |
| % ya Watu wa Kujitolea waliofunzwa walio katika shughuli za kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirika | # ya Watu wa Kujitolea waliofunzwa wanaopeleka ripoti kama inavyotakiwa / # ya Watu wa Kujitolea waliofunzwa kufuatilia watu waliokaribiana na aliyeathirika | Ufuatiliaji wa Programu |
| Idadi ya Jumla ya Wakufunzi (ToT / Mwalimu wa wakufunzi) waliofunzwa Kufuatilia Watu Waliokaribiana na Aliyeathirikana na Idadi ya Jumla ya Wanaojitolea waliofunzwa kufuatilia watu waliokaribiana na aliyeathirika | *Hakuna hesabu inayohitajika* | Inahitajika kwa mahesabu ya ufuatiliaji wa programu na ukaguzi |

## ZANA ZA ZIADA & MWONGOZO

1. IFRC GO kwa mwongozo wa karibuni juu ya ugonjwa wa Coronavirus (COVID-19) pamoja na mwongozo wa afya ya jamii
2. Unyanyapaa wa kijamii unaohusishwa na COVID-19: Mwongozo wa kuzuia na kushughulikia unyanyapaa wa kijamii . (IFRC, WHO, UNICEF)
3. Mazingatio ya WHO katika uchunguzi wa visa na mkusanyo wa COVID-19
4. Ugunduzi wa WHO wa mapema na utambulisho wa COVID-19
5. Zana zote za RCCE na mafunzo, pamoja na ukusanyaji wa maoni na uchambuzi, vinaweza

kufikiwa kupitia muundo wa rasilimali.